**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA NAMTUMBO**

SHULE YA SEKONDARI NANUNGU,
S.L.P 701,
SONGEA.
20/04/2024

MKOA WA RUVUMA
Kumb Na: NNG SS/JI/F5//2024
Headmistress: 0620143783
Second Master: 0621552508
Office No/Mwl. wa Malezi: 0628370909

Mzazi/mlezi wa mwanafunzi …………………………………………………

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI NANUNGU KWA KIDATO CHA TANO MWAKA 2024/2025.**

1. Ninafurahi kukuarifu rasmi kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga kidato cha tano katika shule ya Sekondari Nanungu.
2. Shule hii ipo katika kijiji cha Mlilayoyo umbali wa kilometa moja na nusu kutoka barabara kuu ya Njombe-Songea. Kwa wanaotoka mikoa ya Mbeya, Iringa, Njombe, Dodoma, Morogoro na Dar Es Salaam ambao watapitia njia ya Njombe-Songea watashuka katika kijiji cha Mlilayoyo hapo kuna usafiri wa boda boda kwa nauli ya shilingi elfu moja tu (sh.1000/=) mpaka shuleni. Kwa wale watakaopita njia ya Lindi-Masasi kuja Songea; wasishuke Namtumbo waende mpaka Songea mjini pale watapanda mabasi madogo (Hiace) yanayoenda kijiji cha Mlilayoyo kwa nauli ya shilingi elfu moja tu (sh.1000/=) na pale watachukua boda boda kwa sh.1000/= mpaka shuleni Nanungu sekondari.
3. Shule itafunguliwa tarehe 01/07/2024 kwa muhula wa kwanza. Mwisho wa kuripoti shuleni kwa wanafunzi wa kidato cha tano itakuwa ni tarehe 20/07/2024 ikiwa mwanafunzi hatofika katika muda huo ni wazi atakuwa ni mtoro na hatua za kisheria zitafuatwa.

4. **MOTO WA SHULE: "EDUCATION FOR LIBERATION"**

**MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**

1. **SARE ZA SHULE.**
   - i. Mashati mawili (02) rangi nyeupe tetroni mikono mirefu.
   - ii. Sketi mbili (02) rangi ya **DAMU YA MZEE** mshono wa rinda box isiyo na V pembeni marinda madogo madogo ziwe ndefu mpaka kwenye kifundo cha mguu.
   - iii. Sweta rangi ya **DAMU YA MZEE** lenye shingo ya **"V".**
   - iv. Tai rangi ya **DAMU YA MZEE**.
   - v. Hijabu nyeupe kwa wanafunzi wa kiislamu.
   - vi. Fulana nyeupe ya kuvalia kwa ndani
   - vii. Jozi mbili (2) za viatu vya ngozi vyeusi visivyo na visigino virefu na vya kufunga kamba.
   - viii. Jozi zaidi ya mbili za soksi nyeupe ndefu (stocking )
   - ix. Nguo za kazi ni magauni mawili (02) rangi ya **KIJANI** ya heshima yasiyobana mshono wa solo marefu kufikia enka ya miguu (kifundo cha mguu).
   - x. Kwa wasichana wa kiislamu vazi la Msikitini ni hijabu nyeupe isiyo na urembo (lesi) nusu kanzu tetroni isiyo angaza **LIGHT BLUE** na suruali pana rangi ya **LIGHT BLUE.**
   - xi. **Nguo za michezo:** raba na jezi (bukta ndefu kufikia magotini isiyo bana na t-shirt) rangi nyeusi ( isiwe na maandishi).
   - xii. Track-suit rangi ya **KIJANI** ufito mweupe ni lazima iwe pana tafadhali.
   - **xiii.** **T- Shirt** ya bluu yenye kola nyeupe na ufito mweupe mikanoni (form six) yenye nembo ya shule inayovaliwa siku ya Jumatano na Ijumaa. Unawaeza pia kuipata shuleni kwa ghalama ya Ths 15,000/=.

2. **MICHANGO YA SHULE**

Michango inayotakiwa kulipwa na kila mzazi kwa mwaka ni:-

(i) Mchango wa uendeshaji wa shule Tsh. 65,000/=
(ii) Tahadhari Tsh. 5,000/=
(iii) Nembo Tsh. 5,000/=
(iv) Kitambulisho cha shule Tsh. 5,000/=

**Jumla Tsh. 80,000/=**

**ANGALIZO:**

**1.** Fedha zote zilipwe kwenye Akaunti Namba ya shule: **61802301312** katika Benki **ya NMB. JINA LA AKAUNTI NANUNGU SECONDARY SCHOOL.**

2. Tafadhali andika jina la mwanafunzi na mchepuo kwenye Pay Slip. **FEDHA TASLIMU ZA MICHANGO TAJWA HAPO JUU HAZITAPOKELEWA SHULENI.**

**3 KWA MWANAFUNZI ASIYE NA BIMA YA AFYA (NHIF) AJE NA KIASI CHA TSHS.50,400/= KWA AJILI YA KUPATIWA BIMA YA AFYA (NHIF) KWANI NI MUHIMU SANA. FEDHA HII UTALIPA UKIFIKA SHULENI USIWEKE KWENYE AKAUNTI YA SHULE.**

**MAHITAJI MUHIMU AMBAYO MWANAFUNZI ANAPASWA KULETA SHULENI:-**

(a) **MAHITAJI YA BWENINI**

i. Godoro futi mbili na nusu kwa sita
ii. Mto
iii. Foronya mbili za mto rangi ya light blue.
iv. Chandarua moja kujikinga na Mbu
v. Shuka mbili za rangi ya light blue
vi. Blanketi

(b) **MAHITAJI BINAFSI**

i. Kandambili za kuogea
ii. Ndoo ndogo lita kumi yenye mfuniko
iii. Sabuni za kufulia na kuogea
iv. Tranka (Sanduku la chuma/bati)
v. Mswaki na dawa ya meno
vi. Taulo
vii. Kitenge/Kanga pisi mbili. (Vikio na mitandio haviruhusiwi)
viii. Nguo za ndani za kutosha.

(c) **VYOMBO VYA CHAKULA**

i. Sahani
ii. Kikombe
iii. Bakuli
iv. Kijiko

(d) **VIFAA VYA USAFI NA ELIMU YA KUJITEGEMEA**

i. Dawa ya kusafishia choo lita tano (05) kwa mwaka.
ii. Jembe jipya lenye mpini.
iii. Mifagio ya Chelewa miwili (02) iliojaa vizuri isiyo na mishiko ya miti.
iv. Fagio laini (soft broom) moja
v. Sqeezer moja
vi. Fyekeo jipya lililonolewa
vii. Ndoo kubwa moja lita 20

**Vifaa hivi viletwe na wanafunzi wote.**

**Pamoja na hayo;**

**i.** Wanafunzi wa mchepuo wa **CBG** wanapaswa kuleta reki moja
**ii.** Wanafunzi wa mchepuo wa **HGL** wanapaswa kuleta fagio gumu (hard broom)
**iii.** Wanafunzi wa mchepuo wa **HGK** wanapaswa kuleta panga moja.
**iv.** Wnafunzi wa mchepuo wa **HGFa** wanapaswa kuleta brashi ya choo.

(e) **MAHITAJI YA KITAALUMA**

i. **Ream paper A4** moja kwa muhula.
ii. **Faili mbili (02).**
iii. **Scientific Calculator function fx-991 MS. (Mhimu)**
iv. Graph pad nne (04).
v. Daftari (counter book) zisizopungua 12.
vi. Kalamu za wino na risasi za kutosha
vii. **Dissecting Kit na Dissecting dish with wax kwa wanafunzi wa Biology**.
viii. Mathematical set (**Mhimu)**
ix. Rula ya sentimeta 30.
x. Kamusi ya kiingereza-Kiswahili kwa wanafunzi wa masomo ya lugha **(Mhimu)**
xi. Begi la kubebea madftari.
xii. Daftali nyingine ndogo kumi (10) kwaajili mazoezi na kujisomea.

(f) **MAHITAJI MENGINE YA KUZINGATIA KWA AJILI YA USAJILI**

- Nakala ya cheti cha matokeo (Result slip) ya form four.
- Nakala ya cheti cha kuzaliwa. (Siyo Affidavit).
- Nakala ya cheti cha uraia kwa wasio watanzania.
- Picha mbili (02) za passport. **(ZIANDIKWE MAJINA YA MWANAFUNZI NA MCHEPUO NYUMA YAKE).**
- Picha za passport za wazazi/walezi zibandikwe kwenye fomu namba Na. 3.

## SHERIA ZA SHULE

Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa Sheria Na.10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, yenye dhamana ya Elimu nchini na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu.

Sheria hizo ni kama ifuatavyo:-

1. Heshima na adabu kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
2. Kushiriki kwa makini kufanya maaandalio ya asubuhi na jioni (Morning and Night preparations).
3. Utii kwa walimu, wafanyakazi wasio walimu na viranja.
4. Kuzingatia ratiba ya shughuli za kila siku za shule.
5. Kuwahi katika kila wito (utii wa kengele).
6. Kuvaa sare za shule darasani, muda wa kazi na michezo.
7. Ni marufuku kutoka nje ya mipaka ya shule bila ruhusa.
8. Hairuhusiwi kutembelea vilabu vya pombe, majumba ya starehe wala nyumba za wageni.
9. Ulevi wa aina yeyote ni marufuku.
10. Ugomvi na matusi ni mwiko.
11. Wizi, kuharibu mali/kifaa cha shule au kuandika maandishi na michoro kwenye kuta z;a shule , milango, n.k ni marufuku.
12. Kila mwanafunzi anatakiwa awe msafi.
13. Ni mwiko kutupa taka/karatasi au uchafu ovyo.
14. Urafiki wa kimapenzi hauruhusiwi shuleni.
15. Ni marufuku kwa mwanafunzi kuolewa au kujiusisha na mapenzi ya jinsi moja.
16. Ni marufuku kwa mwanafunzi kwenda nyumbani kwa walimu/wafanyakazi bila ruhusa.
17. Vazi lingine lolote nje ya sare za shule likivaliwa Shuleni hatua za kinidhamu zitachukuliwa dhidi yako.
18. Hereni, mikufu, pete, shanga, bangili n.k. haviruhusiwi kuvaliwa Shuleni.
19. Hairuhusiwi kupaka rangi kucha, wanja machoni au kujichubua kwa mkorogo .
20. Ni marufuku kwa mwanafunzi kutumia vyombo vya umeme Bwenini/darasani au mahali popote ndani ya shule.
21. Ni marufuku mwanafunzi kuwa na simu ya mkononi shuleni. Adhabu kali itatolewa ikiwemo kulipia uharibifu wa mfumo wa umeme na mzazi kumuhamisha mwanafunzi husika.
22. Kufeli au kutofanya mitihani au kupata "**F**" kwenye mitihani na mazoezi darasani ni kosa lisilovumilika.

## MIIKO MAALUMU

**MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE**

a) Kashifa ya aina yeyote kwa Taifa kama kudharau mambo ya kitaifa (sikukuu za kitaifa, mikutano, wimbo wa Taifa, Bendera ya taifa, maandamano, n.k).
b) Wizi (kuiba)
c) Kuoa au kuolewa.
d) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma/shule.
e) Kutohudhuria shule kwa muda mrefu (utoro) bila taarifa.
f) Kupigana au Kupiga.
g) Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla.
h) Kufanya jaribio lolote la kujiua au kutishia kujiua kama kunywa sumu, n.k
i) Kuchochea ghasia/kugoma au kuongoza migomo na kuvunja amani na usalama wa shule na watu.
j) Kuvuta sigara, kunywa pombe, bangi au dawa za kulevya.
k) Kuendesha magendo au ulanguzi wa aina yeyote.
l) Kosa la jinai, kosa likithibitishwa na polisi au mahakamani.
m) Kulala nje ya shule bila ruhusa.
n) Kugoma adhabu.
o) Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.
p) Uasherati.
q) Kuwa mjamzito (kupata mimba).
r) Kutoa mimba.

**MUHIMU**

(i) **Shule inafuata muhula inayotolewa na wizala ya elimu, hivyo inakuwa na mihula mirefu miwili na mifupu miwili kwa mwaka mzazi/ mlezi unaombwa kutoa ushirikiano wako kuhakikisha mtoto anawasili kwa wakati vinginevyo sheria itachukua mkondo wake.**

(ii) **Mawasiliano yote kati mwanafunzi na mzazi au mlezi yafanyike kupitia mkuu wa shule, makamu mkuu wa shule na ofisi ya malezi na mwanafunzi haruhusiwi kuwa na simu ya mkononi akiwa shuleni.**

(iii) **Aidha unashauriwa kutomruhusu mwanao kumiliki simu kipindi hiki ambacho umri wake unampa shida kuyatawala mazingira ya utandawazi.**

(iv) **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi.**

(v) **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye bweni alilopangwa na kitanda alichopangiwa.**

(vi) **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalumu toka MKUU WA SHULE (akipata msiba au ugonjwa).**

(vii) **Shule inautaratibu wa kushughulikia usafiri kwa wanafunzi wanao toka mbali pindi shule inapofungwa. Hivyo mzazi/ mlezi utapewa taarifa kabla ya shule kufungwa.**
**Shule itakapokuwa imefungwa, likozo zote mwanafunzi atatokea shuleni moja kwa moja kwenda kwa mzazi wake (nyumbani kwao) na shule itakapo fungua atatokea nyumbani kwao (kwa mzazi) moja kwa moja kuja shuleni atakae kiuka utaratibu huu atarudishwa nyumbani kwa gharama zake.**

(viii) **Mwanafunzi anaruhusiwa kuja pasi ya mkaa kwaajili ya kunyoshea nguo zake. Ni marufuku mwanafunzi kuwa na kutumia pasi ya umeme aama kifaa chochote kinachotumia umeme akibainika hatua kali zitachukuliwa dhidi yake ikiwepo kusimamishwa shule.**

(ix) **Mzazi au mlezi kutompa mtoto fedha nyingi zitakazo mfanya apoteze utulivu wa Maisha ya shule na kuvunja sheria za shule.**

(x) **Mzazi anashauriwa akupatie fedha zakutosha kwa matumizi yako binafsi aidha mwanafunzi aruhusiwi kuweka fedha bwenini mkabidhi mhasibu akutunzie, vile vile mzazi au mlezi atume fedha ya matumizi kupitia simu ya shule, namba ni 0628370909 ( jina JUDITH M. NDOMBA) ambayo inatunzwa na mwalimu wa malezi. Mzazi akishatuma fedha kwenye simu ya shule aandike ujumbe kumtambilisha muhusika mfano: Nimetuma Tsh. 23,000/= kwa mwanafunzi JACKRINE MMARI kidato cha tano CBG.**

(xi) **Mzazi hakikisha unapima afya ya mwanao kwa uhaminifu ili kuepuka usumbufu wakati wa masomo.**

(xii) **Iwapo mwanao ana ugonjwa unaomsumbua mara kwa mara tafadhari aje na vyeti pamoja na dawa anazotumia na akabidhi kwa matroni wa shule. Hii itarahisisha shule kumuudumia, usipo fanya hivyoshule itashindwa kumuudumia. Usifiche ugonjwa, utapokelewa tu kupata elimu ni haki yako.**

(xiii) **SIKU YA KUMTEMBELEA MWANAFUNZI NI JUMAMOSI YA MWISHO WA MWEZI TU NA SIO SIKU ZA MASOMO.**

Ni matumaini yetu kuwa mwanao atafurahia maisha na masomo kwa muda wote atakaokuwa hapa na kwamba ataonyesha tabia njema na atakuwa na ari ya kujifunza, pia anahitajika kutekeleza shughuli zote zinazohusu uanafunzi wake kwa juhudi na maarifa.

HITIMISHO

i. Viambatisho (Fomu) Na. 1, 2 na 3 zijazwe kabla mwanafunzi hajaripoti shule. (Aje nazo zikiwa zimejazwa ipasavyo).
ii. Mwanafunzi aje akiwa amevaa gauni la kazi. Nguo za nyumbani haziruhusiwi..
iii. Kuhudhuria vipindi darasani, kufanya majaribio na mitihani na kuhudhuria morning na night preparations ni LAZIMA sio hiari.
iv. Mwanafunzi anapokuwa shuleni muda wote anapaswa kuzingatia utunzaji wa mazingira na miundombinu ya shule na matumizi bora ya vyoo, samani na vifaa mbalimbali vya shule na vya kwake binafsi.

Mwanao anatakiwa daima atii <u>sheria</u>, <u>taratibu</u> na <u>kanuni</u> za shule ili aje avune kile kilichomleta hapa yaani ELIMU.

**HONGERA NA KARIBU SANA**

........................
JUDITH M. NDOMBA
MKUU WA SHULE

MKUU WA SHULE
NANUNGU SEKONDARI
S.L.P 701 SONGEA

**FOMU NA. 1**
**FOMU YA UTHIBITISHO WA MKATABA WA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI NANUNGU NA KUTEKELEZA SHERIA ZA SHULE KWA MWANAFUNZI**

**A: IJAZWE NA MWANAFUNZI**

Mimi……………………………………..nikiwa na akili timamu, Nakubali kuchukua nafasi niliyopewa ya kidato cha tano. Ninaahidi kufuata sheria , kanuni, taratibu na masharti mengine yote ya shule, ikiwemo kutopata **F** darasani, kutomiliki simu ya mkononi shuleni, utoro wa vipindi na mitihani. Naahidi mbele ya mzazi/mlezi wangu kuwa nitajitahidi kwa upeo na uwezo wangu kuwa mwanafunzi mwema, sitashiriki migomo na mambo yatakayosababisha kuachishwa shule. Nitashirikiana na walimu pamoja na wanafunzi wenzangu katika kila jambo lenye manufaa kwa shule na Taifa kwa ujumla.

Jina la mwanafunzi……………………………………

Uraia…………………………………………………..

Dini…………………………………………………….

Kabila………………………………………………….

Tarehe ya kuzaliwa…………………………………….

Saini……………………………………………………

Tarehe ya mkataba……………………………………..

**B: IJAZWE NA MZAZI/MLEZI**

Mimi………………………………..mzazi/mlezi wa mwanafunzi…..……………………………Nikiwa na akili timamu, nimesoma vyema sheria, taratibu na kanuni za shule. Nakubali mwanangu ajiunge na shule ya sekondari Nanungu. Ninaahidi kwamba nitampatia mahitaji yake yaliyotajwa katika fomu ya kujiunga na shule. Endapo mwanangu ataenda kinyume na sheria na taratibu za shule na kupatikana na kosa la kupata **F** kwenye masomo, kumiliki simu ya mkononi shuleni, kushiriki migomo, utoro wa vipindi, kukwepa mitihani kama ilivyoanishwa hapo juu, nakubali sheria ichukue mkondo wake ili kuepusha madhara kwa wanafunzi wengine na shule kwa ujumla wake. Nafahamu fika kwamba kilichomleta shule ni kusoma na si vinginevyo.

Sahihi ya mzazi/mlezi..………………………

Namba ya simu 1..…………………………..
2……………………………(WhatsApp)

Tarehe……………………………………….

**FOMU NA. 2**
**FOMU HII IJAZWE NA DAKTARI WA KITUO CHA AFYA AU HOSPITALI**

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**MINISTRY OF EDUCATION, SCIENCE AND TECHNOLOGY**

Nanungu Secondary School,
P.O.Box 701,
Songea.
……………………

TO MEDICAL OFFICER
…………………………………….
…………………………………….
…………………………………….

**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

Please examine Miss……………………………Form ………Combination……………As to her fitness for pursuing secondary school studies in this school.

1. Vision with/without glasses right …………………………… Left …………………….
2. Blood pressure ………………………………… hemoglobin ………………………
3. Hearing ………………………………………................................................
4. Urine (a) Albumen ………………………………. (b) Sugar …………………………
5. Stool ……………………………………………………………………………
6. Blood group ……………………………………………………………………
7. (a) Venereal Disease ………………………………….. (b) Bilharzia ………………
8. Pregnancy……………………………………………………………………
9. Neurosis ……………………………………………………………………
10. Is there any abnormality of:
   (a) The heart ……………………………….
   (b) Speech …………………………………
   (c) Others …………………………………..
11. Are there any serious disease e.g. Leprosy, Asthma, Diabetes etc ………………………..

Additional information if any ……………………………….........................................

Date ……………. Name and Signature of Medical Officer…………………………………….

Station ……………………………….. Designation ………………………………

**FOMU NA. 3**

**TAARIFA ZA NDUGU WATAKAOFIKA KUMUONA NA KUSIKILIZA SHIDA MBALIMBALI ZA MWANAFUNZI**

**JINA LA MWANAFUNZI………………………………………………………..**
**KIDATO CHA ………………………..MCHEPUO WA…………………………**

**PICHA ZA WAZAZI/WALEZI WAWILI ZIBANDIKWE HAPA**

**A. NDUGU WA KUMTEMBELEA NA KUSILIZA SHIDA ZA MWANAFUNZI**

1. JINA…………………………………………………………………………….
   JINSI……………………..KABILA……………………………………….
   ANAKOTOKA……………………………………………………………
   UHUSIANO WAKE NA MWANAFUNZI………………………………..
   NAMBA YAKE YA SIMU…………………………………………………

PASSPORT

2. JINA…………………………………………………………………………….
   JINSI……………………..KABILA……………………………………….
   ANAKOTOKA……………………………………………………………
   UHUSIANO WAKE NA MWANAFUNZI………………………………..
   NAMBA YAKE YA SIMU…………………………………………………

PASSPORT

3. JINA…………………………………………………………………………….
   JINSI……………………..KABILA……………………………………….
   ANAKOTOKA……………………………………………………………
   UHUSIANO WAKE NA MWANAFUNZI………………………………..
   NAMBA YAKE YA SIMU…………………………………………………

PASSPORT

**B. MZAZI AWAIDHINISHE HAO NDUGU WA MWANAFUNZI**

MIMI…………………………………….MZAZI/MLEZI WA
MWANAFUNZI………………………………………………………………

NINAWAIDHINISHA WATAJWA HAPO JUU KUWA NI NDUGU WA MWANANGU NA WATAKUWA WAKIFIKA KUMUONA NA KUSIKILIZA SHIDA MBALIMBALI WAKATI AMBAO MIMI KAMA MZAZI/MLEZI NITAKUWA NIMESHINDWA KUFIKA

SAINI……………………………………

NAMBA YA SIMU……………………………….TAREHE………………………………………

**C. KIONGOZI WA SERIKALI YA MTAA/KIJIJI ATHIBITISHE TAARIFA HII**.

MIMI………………………………………………CHEO……………………………………

MTAA/KIJIJI………………………….

NATHIBITISHA HAPO JUU WAMETEULIWA NA MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI NA NINAKUOMBA WAWE WALEZI MBADALA WA MWANAFUNZI TAJWA HAPO JUU

SAINI…………………MUHURI……………………………TAREHE…………………………

NAMBA YA SIMU……………………….

**ORODHA YA VITABU AMBAVYO MZAZI ANAWEZA KUVINUNUA KWA AJILI YA MWANAE ILI AJISOMEE YEYE BINAFSI**

**CHEMISTRY**

(i) Advance level organic by APE network 2012"
(ii) A' level secondary Education chemistry practical
(iii) Advance inorganic chemistry volume I and II by S. CHAND
(iv) Environmental chemistry and pollution control by S. CHAND
(v) Essential physical chemistry by S. CHAND
(vi) Selected topic in inorganic chemistry by Wahid .U. Malik et at
(vii) Organic Chemistry by S. CHAND.

**BIOLOGY**

i) CJ CLEGG with DG MACKEAN (2000) Advanced Biology principle and Application 2nd ED, Hodder Murray London.
ii) Sylvia S Mader (1996), Biology (5th ED) Wm C, Brown Publisher London
iii) DJ Taylor et al (1997), BIOLOGICAL SCIENCE, Cambridge University press – New York.
iv) MBV Roberts (1986), Biology A functional Approach (4th ED)
v) Ann Fullick et al (2011), A level Biology, students Books, Longman

**BASIC APPLIED MATHEMATICS**

- Basic Applied Mathematics For Advanced Secondary Schools Form V by Septine I. Sillem
- Basic Applied Mathematics For Advanced Secondary Schools Form VI by Septine I. Sillem
- Basic Applied Mathematics for Advanced Level Secondary Schools student's Book Form Five and Six by TIE

**GENERAL STUDIES**

i) General studies for Level Certificate form V BY. RICHARD MBALASE
ii) General studies for A'level certificate from VI. BY RICHARD R. MBALASE.

**GEOGRAPHY**

i) Practical geography Alive By Zisti
   - Map Reading, photography interpretation, Field Research, Statistics, and survey by Ellis Anthony Mkoko.
   - Affordable Edition for Secondary and High School learners kot publisher
ii) A comprehensive approach to physical and high school learners kot publisher.
iii) Human and economical geography by GILLAN .C. MARGAN
iv) Soil and climatology by zisti.
v) Principle of Physical Geography by F.J Monk House
vi) Geography integrated approach by: D. Waugh
vii) General geography in diagrams by R.B Burnet
viii) Statistical methods and the Geographers by S. Gregory
ix) Geography 1 & 2 questions with answers (Review) by Msabila / Nyambari.

**HISTORY**

i. Modern World History by Ben Walsh
ii. African in the World History by Nyirenda
iii. The Russian Revolution and the Bolshevik Victory by D.C Heath and company
iv. Major events in the African History by Fr. Kamara.

**ENGLISH LANGUAGE 01**

i. Mgonja M.E. (2019). "The Comprehensive Linguistic: English language for form 5&6. Nice Enterprises
ii. Ustaadh Shaban B.O. "Language A Hand book for A-level Secondary Students: Preparation for paper one and two
iii. Nicholaus Asheri (2017). "English Language Structure & Stylistics: A practical Approach". 4th edition. APE Network.
iv. Advanced English Dictionary – Oxford University

**ENGLISH LANGUAGE 02**

i. English for Advanced Level Dr. Kadeghe
ii. Selected poems from East Africa by TIE and other poems text books.
iii. The beautiful ones are not yet born by Ayi Kwei
iv. A man of the people by Achebe
v. Death of sales man – Henry Ibsen
vi. Rwanda Magere – Okoit Omtata
vii. The bride price by Austine Bukenya

**KISWAHILI**

i. Nadharia ya Lugha – Masebo
ii. Nadhari ya fasihi – Masebo
iii. Nadhari ya Lugha – Saluhuya, C.
iv. Mfadhili- Hussein Tuwa
v. Kufikirika- S. Robert
vi. Kivuli kinaishi-E. Hussein
vii. Morani-E. Mbogo
viii. Kimbunga –H. Gora
viii. Fasihi maswali namajibu kidato cha tano na sita – Masebo.
ix. Kamusi ya Kiswahili sanifu.